

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Simu Nambari: 2152532/3

Fax Na: 2152820

(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe
kwa Kamishna Jenerali)



08 Barabara ya Kivukoni
S.L.P. 80327,
11486 DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA UMMA

KAMISHNA JENERALI ATOA SALAMU KWA VYOMBO VYA HABARI

Dar es Salaam, 30 Aprili 2021:

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kamandi ya Wanamaji; tarehe 24 Mwezi Aprili, 2021 majira ya usiku katika Bahari ya Hindi upande wa maji ya Tanzania ilifanikiwa kukamata dawa za kulevya.

Dawa hizo ni **heroin hydrochloride** kiasi cha kilo 504.36 na Methamphetamine kiasi cha kilo 355 ambazo zina jumla ya kilo 859.08, zilizokuwa zimefichwa ndani ya jahazi la uvuvi liliokuwa likitokea Nchini Iran.

Katika Tukio hilo Mamlaka inawashikilia watu saba ambao ni Jan Mohammad Miran (42) ambaye ni nahodha wa jahazi hilo, Amir Hussein Kasom (35), Issa Baluchi Ahmad (30), Salim Baluchi Fedhmuhammad (20), Iqbal Pakil Mohammad (22), Jawid Nuhan NurMuhammad umri miaka 19, na Mustaphar Nowan Kadirkash umri miaka 20.

Watuhumiwa wote ni raia wa **IRAN** na wamefikishwa leo mahakamani kwa kosa la Uhujumu Uchumi, kesi namba 02 ya mwaka 2021 mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Maria Bantulayne na kusomewa mashtaka ya kusafirisha dawa za kulevya .

Ukamataji huu ni mkubwa kuwahi kufanyika Nchini tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya mwezi Februari 2017, na huu ni mwanzo kwani mapambano ndiyo yameanza. Lengo la Mamlaka kuiona Tanzania iliyo huru kutoka kwenye matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha magonjwa mbalimbali yakiwemo ya akili, uraibu, moyo, ini na mapafu. Matumizi hayo pia huchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU, virusi vya homa ya ini na kifua kikuu mionganini mwa watumiaji na jamii kwa ujumla.

Aidha, Matumizi ya dawa za kulevyta husababisha kukithiri kwa vitendo vya kihalifu katika jamii kama wizi, utapeli na uporaji ambayo hufanyika ili kupata fedha za kununulia dawa hizo.

Wafanyabiashara wa dawa za kulevyta huendesha magenge ya utekaji, mapigano na mauaji na kuifanya jamii kuishi kwa woga. Kadhalika, wauzaji wa dawa za kulevyta wana wanajihuisha na biashara nyingine haramu kama usafirishaji wa binadamu ambapo huwaweka watu rehani (bondi), silaha za magendo, meno ya tembo, nk. Wafanyabiashara hawa huweza kuvuruga usalama kwa kufadhili vita na ugaidi.

Kwa upade wa uchumi, dawa za kulevyta huambatana na utakatishaji wa fedha haramu zinazotokana na biashara hiyo ambapo madhara yake ni pamoja na kuhamisha nguvu ya kifedha kutoka kwenye Serikali, masoko na wananchi na kwenda kwa wahalifu ambao ni wafanyabiashara wa dawa za kulevyta.

Kwa upande wa mazingira, Kilimo cha bangi na mirungi hufanyika katika maeneo yasiyofikika kirahisi kama vile kwenye milima, misitu na kwenye vyanzo vya maji na hivyo kusababisha kukauka kwa vyanzo vya maji, ukame, mmomonyoko wa ardhi na kutweka kwa baadhi ya viumbi hai na uoto wa asili.

Madhara dawa za kulevyta ni mengi na makubwa haya yaliyotajwa ni kwa uchache tu. Hivyo, Kwa wale wanaojihuisha au wanaofikiria kujihuisha na biashara ya dawa za kulevyta, wanatakiwa kufahamu kwamba, Mamlaka pamoja na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama, tutafanya kazi usiku na mchana na tutatumia muda wetu na weledi wetu wote kuhakikisha wahusika wote wanakamatwa na kufikishwa mbele ya sheria.

Ni jukumu letu watanzania wote kushiriki katika mapambano haya kwa kutoa taarifa kwa Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na Dawa za Kulevyta juu ya watu wanaojihuisha na biashara ya dawa za kulevyta. Na niwahakikishie kuwa taarifa utakayoitoa itapokelewa na kufanyiwa kazi kwa usiri mkubwa.

Imetolewa na,



Florence Khambi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta.